# Mfumo ulioboreshwa wa kilimo mseto cha mipira

Mfumo ulioboreshwa wa kilimo mseto cha mipira ambao hujulikana kama RAS 1 ni sawa na mfumo wa kienyeji wa kilimo cha mpira ambao wakulima hukuza mpira lakini huruhusu mimea asili kukua katikati ya miti ya mpira.
Katika hili, miti ya mpira wa ubora wa juu hupandwa badala ya miche duni. Katika hili, haja la kupalilia linapunguzwa ikilinganishwa na kilimo cha aina moja ya mmea. Malengo ya mfumo wa RAS 1 ni kupunguza gharama ya uanzishaji wa shamba la mpira huku tija ikiongezwa, pamoja na kutekeleza kilimo-uhifadhi kwa usimamizi bora wa viumbe bai.

## Kuanzisha kilimo cha mpira kilichoboreshwa

Ardhi inayotumika kwa kilimo mseto cha miti ya mpira kilichoboreshwa cha RAS 1 inaweza kutoka kwenye msitu mzee wa mpira, msitu wa pili (msitu ambao umeota tena baada ya kuukata) au vichaka. Katika mfumo huu unaweza kutumia vibarua vya nyumbani, na rasilimali za kifedha zinazohitajika ni chache.
Ili kuanzisha shamba la miti ya mpira, fyeka mimea mirefu iliyo kati ya safu za miti kwa sababu mimea mirefu inaweza kuathiri ukuaji wa miti ya mpira. Pia ondoa magugu na mimea mingine kutoka kwenye safu za miti ya mpira. Aina bora za miti ya mpira zinazofaa kwa mfumo wa RAS 1 ni pamoja na; PB 260, BPM 1 na RRIC 100. Utomvu wa miti unaweza kukusanywa wakati miti inapokuwa na umri wa miaka 5 hadi 7.

## Usimamizi bora wa mipira

Kabla ya kupanda, shamba hutayarishwa kwa kuondoa mimea, na miche kupandwa kwa umbali wa 3m kwa 6m ambao hutoa miti 550 kwa hekta. Baada ya kuchimba mashimo ya kupandia na kupanda miche, zao la mseto kama vile mpunga linaweza kupandwa kati ya miti ya mpira kwa mwaka wa kwanza.
Kupalilia mara kwa mara kunahitajika kwenye safu ya miti ya

mpira. Mbolea huwekwa kwenye miti ya mpira hadi mwaka wa tatu, lakini ikiwa mkulima anaweza pia kuweka mbolea hadi miti itakapoanza uzalishaji.

Kudhibiti magonjwa ya uozo wa shina na uozo wa mizizi, katika miti ya mpira ni muhimu.

Mfumo wa RAS 1hupunguza gharama za vibarua na matumizi ya viuatilifu kwa sababu kupalilia hufanywa tu kwenye safu ya miti, huongeza uzalishaji, husaidia katika uhifadhi wa viumbe hai na hudhibiti mmomonyoko wa udongo.